

## NOTISI YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

**Taarifa inatolewa kuwa, Mkutano Mkuu wa 58 wa wanahisa wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc) kwa mwaka ulioishia Disemba 31, 2022, utafanyika Hyatt Regency Kilimanjaro Hotel, Dar es Salaam Tanzania siku ya Ijumaa Aprili 21, 2023, saa 4.00 asubuhi.**

### Ajenda:

1. Notisi na akidi.
2. Kuidhinisha ajenda
3. Kuthibitisha mhutatasi wa mkutano mkuu wa 57 uliofanyika Aprili 21, 2022.
4. Yatokanayo na mhutatasi wa kikao kilichopita
5. Kupokea na kuthibitisha taarifa ya mahesabu ya mwaka iliyokaguliwa kwa mwaka unaoishia Disemba 31, 2022.
6. Kuidhinishwa gawio.
7. Kuthibitisha wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka 2023.
8. Kustaafu, kujiuzulu na uteuzi wa Wakurugenzi.
9. Kupokea na Kuidhinisha Pendekezo la malipo ya Wakurugenzi Wasiokuwa Watendaji.
10. Mengineyo.

### Muhimu:

1. Mwanahisa anayetaka kuhudhuria mkutano atalazimika kujigharamia mwenyewe. Aidha, mwanahisa huyo lazima aje na nakala ya risiti yake ya amana au cheti cha kushiriki pamoja na kitambulisho chake.
2. Mwanahisa mwenye haki ya kuhudhuria katika mkutano na kupiga kura anaweza kuteua mwakilishi ambaye atahudhuria katika mkutano na kupiga kura kulingana na katiba ya kampuni.
3. Fomu ya mwakilishi lazima iwasilishwe katika ofisi za kampuni si zaidi ya Alhamisi, Aprili 20, 2023 saa 4 asubuhi.
4. Nakala za ripoti ya mwaka kwa mwaka ulioishia Disemba 31, 2022 zitapatikana katika ofisi zilizoajiliwa za Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc) kuanzia Aprili 17, 2023, kwa anwani iliyoonyeshwa hapa chini. Nakala tepe(Soft copy) zinaweza kuombwa kwa kupitia barua pepe ifuatayo: [kabwe.mwenge@jti.com](mailto:kabwe.mwenge@jti.com)
5. Taarifa zaidi kuhusiana na mkutano mkuu huu zinawezakupatikana kwenye tovuti ya TCC Plc ([tcc.tz](http://tcc.tz)).

Kwa amri ya Bodi



Godson M. T. Killiza  
Katibu wa Kampuni  
Kiwanja Namba 20  
Barabara ya Nyerere  
S. L. P 40114  
Dar es Salaam.